


**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI
NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
(NACTVET)**



**UTARATIBU WA KUOMBA UDAHILI WA MKUPUO WA MACHI
MWAKA 2022/2023**

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linapenda kuutaarifu umma kuwa udahili wa Machi umeruhusiwa kwa vyuo vyote vyenye uwezo na uhitaji, isipokuwa vyuo vinavyotoa mafunzo katika kada za **Afya na Sayansi Shirikishi**. Vyuo vyenye uhitaji huo vinapaswa kuandika barua ya maombi na kujaza fomu inayopatikana katika tovuti ya Baraza (www.nacte.go.tz). Maombi yatumwe kupitia Ofisi za Kanda za NACTVET.

Ratiba ya maombi ya udahili wa Mkupuo wa Machi imeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Ratiba ya Udahili kwa Mkupuo wa Machi 2022/2023

TAREHE	TUKIO	WAHUSIKA
18 -22 Machi, 2022	Kuwasilisha barua ya maombi ya Udahili	Vyuo (Wakuu wa Vyuo)
22 - 30 Machi, 2022	Kuchambua Maombi	NACTVET
31 Machi 2022	Kutoa majibu kwa Vyuo vilivyoomba kudahili Mkupuo wa Machi	NACTVET
1-10 Aprili 2022	Kupokea maombi ya Wanafunzi (kwa vyuo vilivyoruhusiwa tu)	Vyuo
11 Aprili 2022	Kuchagua waombaji	Vyuo
12-18 Aprili 2022	Kuwasilisha majina ya waombaji waliochaguliwa NACTVET kwaajili ya uhakiki	Vyuo
18 - 24 Aprili 2022	Uhakiki wa waombaji waliochaguliwa	NACTVET
25 Aprili 2022	Majibu ya Uhakiki	NACTVET
25 Aprili – 25 Mei 2022	Usajili wa wanafunzi waliohakikiwa	Vyuo

**IMETOLEWA NA:
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
TAREHE: 17/03/2022**